# DUNIA ISIYOONEKANA NA YA KIMIUJIZA

*Waebrania 11:1-2. Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo ya Tarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyo onekana. Maana kwa hiyo wazee wetu Walishuhudiwa.*

Sasa, unapopokea uvuvio ya kuwa Yesu Kristo alikufa kwa dhambi zako, ni saa ile ile ambapo uponyaji wako umekuja.
Hiyo ni kweli. Unapopokea kutoka Mbinguni, kwamba Yesu alikufa kwa dhambi zako na umelikubali hilo, huhitaji maombi kwa ajili yako tena. Tayari umelikubali hilo, hilo limemalizika. (2korintho 3:6)

Sasa, tunaweza kuhubiri Neno, kuelezea Neno, lakini inabidi ulipokee lile Neno. Oh, halleluya. Hilo ndilo linaloliwasha moto, ndugu. Unapolipokea hilo, ule ufunuo, kitu fulani kinateleza kutoka ile dunia isiyoonekana ng'ambo, inakuja ikivingirika chini kupitia njia isiyoonekana mahali fulani kwenye nafsi yako; ambayo inasema, "sasa naliona hilo". Macho yako yanang'ara; midomo yako iliyoinama chini, inanyooka mbele na kucheka. Kila msuli katika mwili wako unaonekana ukifurahi. Kitu fulani kinaenda kutokea. Kitu fulani……..
Huhitaji kuwa katika mstari wa maombi tena. Umelipata hilo sasa (Mathayo 16:17-18: Mathayo 11:25-26). [1].

Sasa, ni lini kitabu cha ufunuo kiliandikwa? Kwa mara ya kwanza kiliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Ufunuo 13:8). Na, Yohana, kwa moyo tu uliyojawa na Roho Mtakatifu…. Unaliona hilo?
Viumbe vya kimalaika vikishirikiana pamoja. Oh, natumaini unalipata hilo, hilo limedondoka kutoka juu sasa hivi, bure. Angalia kama una Roho Mtakatifu ndani yako, sasa wewe ni mwanafunzi awezaye kushirikiana na dunia ile isiyoonekana na ya kimiujiza. Siyo ajabu watu hawawezi kuamini mambo haya; bado hawajaweza kukutana.kiushirika. Hawana kitu hapa cha kuaminia.

Lakini Roho Mtakatifu anapokuja ndani ya moyo, haraka anakuwa kiumbe mwenye hali mbili: moja ya dunia itakufa; na moja ya mbinguni itaishi. (Yohana 3:3). Amen. Katika mwili wake bado Yeye anakabiliwa na kifo (2korintho 4:16). Lakini katika Nafsi yake imepita kutoka mautini kuingia uzimani. (Yohana 5:24). Katika mwili wake anao ushirikiano/ mawasiliano na hisi zake tano. Katika Roho yake ana mawasiliano ushirikiano na Mungu kupitia Roho Mtakatifu. Na malaika wa Mungu huwatembelea. (Zaburi 91:11) na kuzungumza nao, ni wajumbe waliotumwa kutoka kwa Mungu ili kufunua, na kuleta ujumbe kutoka kwa Mungu kwa mtu binafsi (Waebrania 1:14)….. Huwezi kuweka chungu kabla msingi haujawekwa. Unaona? Kwa hiyo inabidi tukumbuke hilo, kuweka vitu vya kwanza, kwanza. Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa (Mathayo 6:33-34). [2].

Basi tunaogopeshwa na nini? Yesu yuko hapa. Roho wake yupo hapa (Matayo 28:19-20). Kumetokea nini sasa hivi? Nilienda katika dunia nyingine. Ni dunia isiyoonekana. Tunakuwa na ufahamu hasa tunapoangalia mmoja kwa mwingine kama hivi. Lakini kuna dunia isiyoonekana; na wewe…….. Ni kuu zaidi ya chochote unachokiona (2korintho 12:1-5). Na hapa yuko Kristo.

Katika dunia hii, katika hili jengo hapa kuna Roho ovu na vita. Na wakristo waliopakwa mafuta, na Malaika wa Mungu wakiwazungukia wao (Zaburi 34:7) wakijaribu kuwatia nguvu kwa Imani.

Na nikiwa nimesimama hapa nikijaribu tu kujisalimisha mwenyewe. Na Roho Mtakatifu akiwa anatembea, na hii ndio tuitayo mahali pa kimbinguni (ulimwengu wa roho) ndani ya Yesu Kristo. (Waefeso 2:4-7). Lakini kumbuka, shetani siku zote anafanya hivyo. Mtu fulani mwenye mawazo ya mashaka, wafanyapo hivyo ni Yeye tu akijaribu kuingilia. Lakini wakristo siku zote wanashinda (Warumi 8:35-39). [3]

Wakati Mungu anapozungumza chochote, inabidi ufunge nafsi yako katika Neno lake na kushikilia hilo. Haijalishi yule wa nje anasemaje, Imani yako inaangalia dunia isiyoonekana. [4].

Sasa tunamuona Bwana wetu katika kazi Yake. Kwamba hawezi chochote Yeye mwenyewe (Yohana 5:19-20,30) ila anachomuona Baba anafanya. Alimpa Mungu utukufu wote, kitu ambacho sio cha kawaida, ni kimiujiza. Kila silaha tulizo nazo, ndugu, silaha zetu zote ni za kimiujiza. Hakuna yoyote ya kawaida tuliyo nayo. Lazima tuliamini hilo.

Tunda la Roho ni nini? Upendo, Furaha, Amani, Uvumilivu, Upole, Utu wema, Subira (Galatia 5:22). Sasa, unaenda chini kule kwenye duka la dawa na unininulie robo ya thamani ya subira. Ninaihitaji hiyo. Upendo wa thamani ya Dollar tano ninaweza kuvumilia vitu vingi kama hivyo. Unaona? Unaona. Ni kitu kisichoonekana. Hizo ndizo silaha zetu zote.
Tunasimama katika dunia ya yasiyo-onekana, tukiangalia mambo yasiyoonekana. Na bado kwetu sisi, tunayaona, kwa sababu Imani yetu inayohisi hayo na kusema iko pale. [5].

Na silaha zote za mkristo sasa hazionekani (waefeso 6:13-20) Mkristo anaangalia yale ambayo hawezi kuyaona kiasili/ ya kawaida. (2Korintho 4:18).

Sasa angalia. Hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kuwa Mkristo. Unahitaji kumuamini Mungu, ambaye huwezi kumuona. (Waebrania 11:6; Petro 1:8-9). Uanaona. Sasa angalia angalia hapa. Silaha zote za Mkristo ni Upendo, Furaha, Imani, Uvumilivu, Subira, Upole, Utuwema; Roho Mtakatifu. Unaona? Vitu hivi vyote ni visivyoonekana; ni visivyoonekana. Lakini vile vitu vile visivyo-onekana ndivyo vilivyo na uhalisia; vile vitu visivyo-onekana. [6].

Huwezi kujifanya mwenyewe uamini. Ni uwezo ambao uko ndani (Waefeso 2:8). Imani ni hakika, siyo kitu chakujifanya, kufikiria (Waebrania 11:1). Ni hakika ya mambo yatarajiwayo. Ni bayana ya mambo unayoamini na huyaoni.

Kwa mara nyingine: Na siliaha zote za Mkristo, sasa kumbuka, ni kwa Imani, zote ni za kimiujiza. Upendo, Furaha, Amani, Uvumilivu, hizo ndizo silaha zote za Mkristo. Mkristo siku zote anaangalia mambo hayaonekani kwa sababu anaangalia ahadi (Warumi 4:13-22). [7].

Ahadi kwa mwaminio ni uzima, Furaha, Amani, Uvumulivu, utu wema, Subira, tunda la Roho, uponyaji wa kiungu, dazeni ya vitu, nilivyo viandika hapa, ambavyo ni miliki yako. Ni vya kwako. Lakini huwezi ukavipata mpaka mmevipigania. (1 Timotheo 6:12). Ni vyako. Kila kitu kinachoonekana, kila kitu kila kitu cha muda kinachoonekana ni changu. Mungu amenipa hicho. Kwa sababu kupitia Kristo Amenipa hicho. Na vitu visivyo-onekana ni vyangu. Amen. Ninapenda hicho. Kile unachoweza kuona, kama uponyaji wa kiungu na kadhalika. Kama hivyo hivyo ni vizuri, tunashukuru hilo; lakini visivyoonekana……….

Sasa, sayansi inaweza kujaribu hapa na kusema, vema hebu tuone; hebu nimchukuwe huyu mtu. Ulisema umeponywa, hebu nimchukuwe na nimfanyie uchunguzi. Hebu nione nini kimetokea. Na kusema ulikuwa na tezi hapa, Bwana?

“Ndiyo, hapo hasa”

“Vema ngoja nikufanyie uchunguzi wa kisayansi na nione kama siyo tu limezama ndani na halikuondoka. Unasema ulikuwa kwanza kipofu na sasa unaona. Nitajuaje? Niache mimi niangalie kisayansi nione hilo”

sasa wanaweza kuchunguza juu ya hilo, lakini bado ni mrithi pia wa kila kitu kinachoonekana (1Korintho 3:21-23). Na halafu ni mrithi pia kwa mambo ambayo hayaonekani, mahali ambapo sayansi haiwezi kuchunguza Amen. Amen. Vitu visivyo-onekana (Amen). Ni mrithi wa hivyo. Ndiyo Bwana. Vitu vile viwezavyo kuonekana. Ni mrithi kwa hivyo. Hii dunia yenyewe ni mrithi wake, wewe ni mrithi. Kila mwaminio ni mrithi; yeye ni mrithi wa hivyo. Vema, halafu yasiyoonekana……… mmiliki wa nini? Mbingu na nchi. Amen. Mambo yote. Unaamini hilo?

Unasema “ndugu Branham, vipi kule nje ambako huwezi kuona? Unajuaje?”. Bado ni vyangu. Amen. Mbingu ni miliki yangu. Hiyo ni sawa. Ni yangu. Mungu amesema hivyo. Na hiyo ni sawa. “Vema, kamwe hujaona, unajuaje iko pale? Najua iko pale kwa vyovyote; Mungu amesema hivyo. Unajuaje ni mrithi wa hiyo, wakati hujaiona kamwe? Naamini Neno lake. Amen. Unaona? Ni mrithi, wewe ni mrithi pamoja na mimi; sisi tuwarithi pamoja kupitia Yesu Kristo (Warumi 8:17). [8].

Katika bustani ya Edeni, shetani alichagua kichwa cha mtu kwa kiakili. Mungu alichagua Moyo kwa Imani. Na kama unatembea kwa Imani, inabidi uamini mambo ambayo huwezi kuyaona au ujadili na akili yako. Tunakuondolea mbali kujadili (2Korintho 10:3-6). Mungu anaposema jambo lolote, hatuliangalii hilo kiakili tena, tunaliacha lizame hasa ndani ya mioyo yetu na kuita kitu chochote kinyume na hicho, kana kwamba hakipo (Warumi 4:16-17). Tunaangalia kile ambacho Mungu amesema, Yeye aliyetoa ahadi.

Hapo ndipo ambapo dunia imefungwa leo. Iko kwenye mahubiri ya kiakili sana. Badala ya makanisa yaliyojazwa na Roho yakiabudu katika Roho, wanasikiliza jumbe za kiakili. Na huwezi ukajadili hili. Hakuna hata kidogo njia ya kufanya hivyo. [9]

Ule uzao wa Ibrahim (Galatia 3:7-29) hauangalii chochote cha mambo ya kiasili; /kawaida wanaangalia kile Mungu alichosema. Hiyo ni ahadi. Ni vipi kama Ibrahimu angeangalia yale ya kiasili/kawaida, kwa mwanamke aliye na miaka mia moja alikuwa na tisini, naye (Ibrahimu) alikuwa na mia moja, na ameishi naye tangu akiwa msicha na alikuwa kijana mdogo na hana uzao? Hakuangalia mambo hayo. Alisema aliyahesabu mambo hayo kana kwamba hayapo, kwa maana aliangalia tuu kile Mungu alicho sema. “Nitakubariki we, Ibrahim, na nitakupa uzao kupitia sarah”.(Mwanzo 17:15-22). Tunaangalia kile Mungu amesema. Mungu amesema hilo, hilo linamamliza hilo [10].

Bado Ibrahim alikuwa na haki ya ile ahadi, na ahadi ilikuwa ni yake, Bado ilibidi apigane ili aweze kuimiliki. Amen. Uko hapo. Mwamini leo, bado tu warithi wa mambo yate, bado tuwarithi wa kila ahadi ya kiroho, kila baraka ya vinavyoonekana, kila baraka ya kilicho ahidiwa na Biblia, bado inadibi upiganie kila inchi ya hilo. Hivyo ndivyo Mungu alivyoiweka, ameipanga hivyo. Siku zote imekuwa hivyo. Inabidi upigane ili umiliki kile unachojua ni cha kwako. Inabidi upigane ili kumiliki hilo. Na hivyo ndivyo tupaswavyo kufanya sasa. [8]

Sasa, unawezaje kuokolewa? Hebu tulichukuwe katika hali ya kitoto ambapo kila mwaminio, haijalishi uko kanisa gani. Na mchungaji wako, kama ni mtu sahihi, atakuambia kwamba unaweza tu kuokolewa kwa njia ya

Imani. Siyo kupitia matendo, kupitia Imani (Waefeso 2:8-9) sasa unaamini kwamba Amekuokoa wewe.

Sasa kitu cha kwanza ambacho kinakuja kutoka moyoni. Unaliamini hilo. Halafu unatembea na kumiliki hilo (Warumi 10:10-13). Useme, “Namkubali Yesu kama mwokozi wangu Binafsi. Ninaamini ameniokoa mimi”. Hakuna kitu kinachoonekana cha dunia hii ambacho kinaweza kuthibitisha kwamba umeokolewa. Macho yako ni rangi ile ile, una shati lile lile ulilokuwa umevaa. Unaenda nje lile kundi la zamani linasema “Hicho siyo chochote kwao” lakini unaamini kuna kitu fulani katika hilo, ni hivyo?

Sasa vipi kama unasema, “Vema nitaenda kuona vile linavyotenda kazi”. Halita tenda kazi mpaka uache ushuhuda wako uendelee (2Korintho 4:13)

Uamini umeokolewa. Utende kama aliyeokolewa. Unasema umeokolewa, Na unashirikiana na wale waliookolewa, na inatenda kazi ya wokovu. Hiyo ni sawa?

Na jambo hilo hilo litafanyika katika uponyaji wa kiungu unaamini umeponywa (1Petro 2:24). Unatenda kama amekuponya wewe. Unasema umeponywa. Na yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yetu kuyafanya yawe mazuri jambo lolote ambalo umelikiri kwamba Yeye amelitenda mbele za Baba (Waebrania 4:14-16). Hilo hapo. [11]

Muda fulani uliopita nilikuwa na fanya mkutano kule kanada. Na nilitembea kule barabarani na kulikuwa na mtu anauza televisheni. Na walikuwa na kipindi wanaangalia kutoka huku Amerika, na alikuwepo kauboy akipiga gitaa. Na huyo mtu akasema, “ningependa nikuulize hii set rafiki”

Nikasema mimi, “umepita tu” oh nikasema “Niko hapa katika huduma” oh akasema, “wewe ni mmoja wao na hili kundi lilillo hapa la Branham”? nikasema ndiyo Bwana ni mmoja wao. Na akasema, “Unafikirije juu ya huyu mtu”? vema hakukuwa na chochote ningeweza kusema kwa wakati huo; Nikasema “oh, nafikiri hii mikutano ni mizuri” Nikasema ulikuwepo pale usiku wa jana? Akasema, Ndiyo “nilikuwepo”. Na nikasema, “unafikirije juu ya mtu yule aliyeponywa aliyekuwa kitandani yule askari, ambaye jina lake liliitwa na akaambiwa yeye ni nani na kuwa amekuwa mgonjwa kwa miaka” “oh” akasema sifikiri chochote juu ya hilo. Kwa sababu nataka kuona ikithibitishwa. Ile hali ya kupumbaza akili (Hypotism) haikubaliani nami. Na unajua, mama yangu mzee wa kusini alikuwa na usemi, mpe ng’ombe kamba ya kutosha, naye atajinyonga mwenyewe” Na nikasema “kwa nini unakuwa…..”

Akasema, “chochote ambacho hakiwezi kuthibitishwa kisayansi, nafikiri hicho siyo chochote” Lakini nikasema. Sitaki kuwa tofauti, lakini inabidi niwe sasa. Mambo ambayo yanaweza kuthibitishwa kisayansi siyo halisi. Ni yale tu ambayo hayakuthibitishwa kisayansi ndiyo halisi.

Oh akasema huu ni upuuzi/dhihaka

Na nikasema vema, nataka nikuulize jambo fulani. Unaweza kuniambia upendo ni nini? Nenda kwenye duka la dawa na unininulie thamani ya robo ya upendo; nauhitaji kiasi, unaona? Huwezi ukauona huo, Ni usiyoonekana. Nionyeshe mimi uhai ni; nahitaji uhai kidogo je unaweza kwenda kuninunulia thamani ya robo? Nionyeshe uhai ni nini. Mungu ni nini. Ni vile vitu visivyo onekana ambavyo ni halisi na vyakudumu. Hivi vitu ni vya muda na vinaharibika. Na bado tunaweka mkazo mkubwa na kushughulishwa na mambo ya asili/kawaida na kidogo sana juu ya mambo ya kiroho.

Na nikasema, “kwa mfano hapa chum,bani tulipo zinakuja picha za televisheni hapa hapa”. Na nikasema, “Inapasa unionyeshe hiyo picha”

Oh akasema ni lazima ipige kwenye hiki chombo na halafu kupitia mrija na kadhalika na inaonyesha hiyo picha hapa. Lakini nikasema, “Huyu mtu yuko kule Amerika”. Na nikasema unachukuliwa kutoka hapahapa, ikija hewani ambapo huwezi kuiona. Akasema, lakini tunaweza kuthibitisha hilo kwasababu picha inaonekana kwamba ipo hapa. Na kiko kituo kinacho thibitisha ipo hapa”

Nikasema, ndiyo, na tunaweza kulithibitisha hilo pia. Kwa maana kule utukufuni tunaye mwokozi aliye fufuka ambaye analituma huku, na Roho Mtakatifu analifunua na kulifanya halisi (chanya). Kwa hiyo tunacho kituo kinachotuma na kituo cha kupokea. Hiyo ni sawa. Mungu mbinguni ajuye mambo yote, anaweza kuweka kipawa katika kanisa lake ili akikuze hicho na kimuakisi Yeye kupitia hicho, na kusema mambo ambayo ni vigumu kuyathibitisha kisayansi. Unaona, hatutembei kwa mambo tuyaonayo; tunatembea kwa mambo tusiyo yaona. [12].

Na kadhalika Mungu yuko hapa na Malaika. Na siku moja itakuwa halisi sana kama vile televisheni au chochote kile, kwa sababu Roho atatuletea sisi katika yale maisha yasiyo na mwisho/ (ambapo hatufi). Hapo sasa tutaelewa. [13].

Na katika ile dunia kuu isiyoonekana ambayo sasa hivi inatuzunguka, inainua hisia zetu kuenda kwenye toba, na kuleta uovu mbele ya mambo yetu, ambayo tumeufanya ni makosa, kwa mioyo ya majuto tunajisalimisha njia zetu ovu, na kuomba huruma za kiungu. Na hebu Roho mtakatifu ambaye ametuonyesha huruma, ampe kila mmoja wetu kadiri tunavyo sihi na kumuomba Mungu atimize Neno lake na kufinyanga maisha yetu na tabia zetu zikubaliane na Neno lake. [14].

Nukuu za kiingereza:

[1] Njia ya Mungu aliyotupa ya kuponywa (54-0719A0Aya E-29

[2] Ufunuo kitabu cha alama(56-0617), Aya 54-55
[3] Imani (56-0815) Aya E-94
[4] Uhai ndio uponyao (57-0611). Aya 44
[5] Haikuwa hivyo tangu mwanzo (62-0630B) Aya E-25
[6] Bwana tunataka kumwona Yesu (62-0724) Aya E-45
[7] Kumwita Yesu katika tukio (64-0319)AyaE-5
[8] Kumiliki mambo yote (62-0506) .Aya 83-87.59
[9] El Shaddai (59-0416).Aya E-19
[10] Kumiliki malango ya adui (59-1108) Aya 42
[11] Udhihirisho wa Roho (51-0717) Aya E-21
[12] Kuyaangalia yale yasiyoonekana (59-0410) Aya E-16-E-18
[13] Wakati wa mavuno (64-1212).Aya 78
[14] Mungu hulishika neno lake (57-0120E). Aya E-83.

*jiwe la kiroho la kujengea na 177 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*